***JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA***

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA**

Shule ya Sekondari Rugambwa,
S.L.P. 357,
**BUKOBA.**

**Tarehe…………**

***Namba za simu**:*
*Mkuu wa shule – 0623610088*
*Makamu Mkuu waShule - 0759813425*
*Matron/Patron- 0756882895*
*Mama Malezi  -0767665844 / 0786665616*

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………........................................................**

**S.L.P ………………………………….......................................................**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI RUGAMBWA HALMASHAURI YA BUKOBA MKOA KAGERA MWAKA……...**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka …….. na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Rugambwa ipo umbali wa Kilometa 5 Magharibi mwa Mji wa Bukoba. Usafiri wa taksi kutoka Bukoba mjini hadi shuleni  haizidi sh. 5,000/=  na usafiri wa pikipiki si zaidi ya  sh. 1500/=.

Muhula wa masomo unaanza **tarehe ………….** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni **tarehe …………….** mwisho wa kuripoti ni **tarehe …………….**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

(i) Shati nyeupe 2 **aina ya tomato (SIYO HALUA)** zenye mikono mirefu na zisizo na urembo wowote.

(ii) Soksi nyeupe jozi 2 (**siyo stocking**).

(iii) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi, vyenye kufunika miguu na visivyo na urembo wowote, jozi 2.(**Siyo mfano wa buti na visiwe na shingo**)

(iv) Nguo za michezo ambazo ni "track suit" ya bluu kitambaa kizito kisichoteleza, isiyo bana na isiyo na kofia (**Adidas**) (picha imeambatanishwa) na raba nyeupe (**Siyo mfano wa buti na visiwe na shingo**), jozi moja.

(v) Sweta rangi ya kijivu shingo ya "V" yenye michirizi myekundu miwili shingoni, mikononi na kiunoni ikiwa na nembo ya shule upande wa kushoto (picha imeambatanishwa).

(vi) Tai yenye michirizi myekundu na myeusi(Za dukani). (Picha imeambatanishwa)

(vii) Sketi nyekundu mbili (2), kitambaa kizito (Esteem) yenye mshono wa "malindabox" jumla ya malinda yawe kumi, mbele matano (5) na nyuma matano (5) na michirizi miwili ya kitambaa cheupe cha tetron inalala kwenye linda la katikati mbele. Upana wa mchirizi ni nusu inchi na nafasi kati ya mchirizi na mchirizi ni nusu inchi. Sketi iwe ndefu ya kufunika miguu hadi kwenye kifundo cha chini cha mguu (picha imeambatanishwa).

(viii) Nguo za nje ya darasa (shamba dress) Gauni 2 rangi ya kijivu (Grey) kitambaa cha tetron nzito au Esteem na siyo aina nyingine ya kitambaa. Mshono wa soro na shingo ya duara; Gauni iwe ndefu inayofunika miguu hadi kwenye kifundo cha chini cha mguu (picha imeambatanishwa).

(ix) "T- Shirt" mbili (2) rangi nyeupe yenye kola isiwe na maandishi Wala alama yoyote (**form six**) kitambaa kizito yenye nembo ya shule upande wa kushoto na nyuma mgongoni. (Picha imeambatanishwa).

(x) Rangi ya hijab (kijuba) ni cheupe na cheusi ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (Picha imeambatanishwa).

**TANIBIHI: Mwanafunzi aje amevaa mojawapo ya sare za shule tajwa hapo juu, asije na nguo yoyote ya nyumbani.**

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

(i) Madaftari makubwa yasiyopungua 10 (counter books quire three)
(ii) Mkebe wa Hisabati (Mathematical set)
(iii) Rula, kalamu za wino na pencil za kutosha muhula
(iv) Dictionary/Kamusi (kwa wanafunzi wa sanaa)
(v) Karatasi (Photocopy papers-double A) Ream 2 kwa mwaka.
(vi) Scientific Calculator na stop watch (wanafunzi wa sayansi)
(vii) Graph pad yenye kurasa 50 (kwa wanafunzi wa sayansi na Geografia)
(viii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
(ix) Mwavuli wa mvua mmoja (1).
(ix) Mto mmoja (1) na foronya mbili (2) za rangi ya pinki.
(x) Mashuka mawili (2 ) ya pinki yasiyo na maua na blanketi moja (1).

(xi) Godoro moja (1) la futi 2½ na chandarua kimoja (1)
(xii) Nguo ya kulalia (**night dress**)
(xiii) Jozi moja (1) ya kitenge.
(xiv) Sahani 1, bakuli 1, kikombe 1, kijiko 1, vyombo vyote viwe vya bati.
(xiv) Toilet papers (karatasi za chooni) kumi (10).
(xv) Kifaa cha kutunzia maji ya kunywa.
(xvi) Taulo moja (1).
(xvii) Nguo za ndani (gagulo /underskirt) chupi za kutosha na sidiria 3.(nyeusi au nyeupe).
(xviii) Taulo za kike zisizopungua paketi 6.
(xix) Sabuni, mswaki, dawa ya meno,mafuta ya kujipaka, dawa ya viatu.
(xx) Ndoo ya kuchotea maji yenye ujazo wa lita 20 na beseni moja la kuogea
(xxi) Box file kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake za mitihani (mali ya mwanafunzi)
(xxii) Fedha za matumizi binafsi. Shule hutoa chakula, mpatie binti yako fedha kidogo kwa ajili ya matumzi yake ya kawaida awapo shuleni. Fedha nyingi humfanya ashindwe kufuata masomo ipasavyo.
(xxiii) Mwanafunzi ni lazima aje na bima ya afya na iwe ni bima inayofanya kazi sehemu yoyote kama HANA aje na **Tshs. 50,400/=** zitalipwa kwenye taasisi ya bima ili akatiwe bima.
(xxiv) Vibanio vya nguo vya kutosha.
(xxv) Kila mwanafunzi aje na taa ya sola kwa matumizi yake binafsi umeme unapokatika.

- **Hakikisha vifaa vyako vyote vimewekewa alama ili kuondoa upotevu.**

**2.3 Vifaa vya usafi.**

Ili kuwafundisha na kuwajengea wanafunzi wetu tabia ya utunzaji wa mazingira na pia kuweka shule katika hali ya usafi na mazingira ya kuvutia, mwanafunzi afike shuleni akiwa na vifaa vifuatavyo:-

| S/N | KIFAA | TAASUSI HUSIKA |
|---|---|---|
| 1. | Panga lililonolewa na fyekeo lililonolewa | **PCM** |
| 2. | Jembe lililonolewa na mpini wake | **HGE na HGFa** |
| 3. | Soft broom yenye mpini na mfagio wa nje (chelewa) na kotama | **HGL** |
| 4. | Hard broom yenye mpini na brash ya sink | **HKL** |
| 5. | Mopper na ndoo yake na squeezer / flaps | **HGLi na PCB** |
| 6. | Mfagio wa buibui wenye mpini wa mbao sio | **HGFa na HGE** |

| | | |
|---|---|---|
| | plastiki. | |

**2.4 Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**N.B.** Fedha hizo zote zilipwe kwenye akaunti ya shule:

**RUGAMBWA SECONDARY SCHOOL Namba ya akaunti 31801100045 Benki ya NMB.**

Mwanafunzi awasilishe nakala ya malipo iliyoandikwa jina lake wakati wa kuripoti.

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepondani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba wa baba/mama, dada/kaka wa tumbo moja au ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;(**shule yetu inaruhusu kusuka kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita tu, aidha mtindo wa kusuka ni nywele za misitari(twende kilioni) isiyozidi mitano bila nyuzi).**
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kupewa taarifa za mwanafunzi pamoja na Namba zao za Simu.
v. Mwanafunzi alete hati ya matokeo (result slip) yake ya kidato cha nne akiwa ametoa „copy‟

**NB: Utumaji wa fedha binafsi za binti yako**
Wazazi wanaowatumia watoto wao fedha za matumizi wafanye hivyo kwa kutumia

njia ya Airtel Money au kwa M-PESA kwenye Namba

**Matron -0756882895 – SIKA MWITA CHACHA),**
**Mama malezi-0767665844/0786665616-MARIANA JOVINUS MUGIZI),**taarifa za kuwataka wanafunzi kufuata fedha zilizotumwa kupitia kwa jamaa zao wanaokaa nje ya shule hazitakubaliwa.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.
JE UNAKUBALI? **NDIYO**☐**HAPANA**☐
(Weka alama ya √ panapohusika)

Jina la Mwanafunzi_______________________ Sahihi _______ Tarehe ______

Jina la Mzazi ______________________ Sahihi _______ Tarehe _________

**NB; Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI NA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO;**

- ***Namba za simu;***
- ***Mkuu wa shule – 0623610088***
- ***Makamu Mkuu waShule - 0759813425***
- ***Matron- 0756882895***
- ***Mama Malezi  -0767665844 / 0786665616***

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**W.K AMOS**
**MKUU WA SHULE.**

ANUANI ...............................
..............................................
............................................

Mkuu wa Shule,

Rugambwa Shule ya Sekondari,

S.L.P. 357,

**BUKOBA.**

**TAARIFA BINAFSI**

A. Jina la Mwanafunzi ....................................................................................................

Anwani ya nyumbani ......................................................................................................

.............................................................................................................................

Kabila ......................................... Tarehe ya kuzaliwa ........./.........../20...........

Mtanzania /Si Mtanzania

Dini ya Mwanafunzi.................. Mtaa/Kijiji ………………… Jina la mratibu elimu kata/mtendaji za…………………simu………......Wilaya....................Mkoa.............

B. Jina la Baba ................................................. * (Hai/Marehemu) .......................

(Mwaka aliofariki) ............................ ………

Dini ya Baba ........................... Kazi ya Baba .......................... Simu Na .................

Jina la Mama ................................................ *(Hai/Marehemu) .............................

(Mwaka aliofariki)..................................

Dini ya Mama ............................ ....... Kazi ............................. Simu Na. .............

C. Taja majina na anuani za Walezi/Ndugu wengine wawili wasiokuwa wazazi wanaoruhusiwa kufika shuleni kusikiliza matatizo ya mtoto na kutoa maamuzi juu ya mashauri ya mtoto wako.

JINA............................................... Uhusiano .......................umri……... SIMU NA. ...............

JINA .............................................. Uhusiano.......................umri……... SIMU NA ……………..

**B.picha za wazazi**

| | |
|---|---|
| | |

**C.picha za walezi**

| | |
|---|---|
| | |

**RUGWAMBWA SECONDARY SCHOOL**
**FORM FOR STUDENT MEDICAL EXAMINATION**

Student"s Name …………………………………………………………………………………

Blood Examination: Haemoglobin …………………………Blood Group ………..

Stool Examination ………………………………………..…………………………………

Urinalysis ……………………………………………………..........……………………

Pregnancy test……………………………………………………………………………...

T.B. Test (If negative, was immunization given)………………………………………..

Eyes…………………………………………………………………………………………

Chest ……………………………………………………………………………………….

Any chronic complaints not noted above e.g.

Asthma …………………………………………………………………………….…

Headache ……………………………………..……………………….……………………

Inability to eat certain foods …………………….. Skin diseases etc....................

Also anything that the School health staff should know about…………………………

……………………………………………………………………………………………………

Any treatment given or recommended ………………………………………………..

**NOTES**: If any of the examinations requested above cannot be carried out, it is useful if it is noted that they have not been done rather than writing NAD down. In case of Bilharzia it is recommended that students attend the Bilharzia clinic before they come to school.

Signature of Examiner ……………………… Designation …

Designation ……………………………………..

Date……………………………………………














RUGAMBWA
GIRLS SEC. SCHOOL